HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA
MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA UJENZI UCHUMI NA MAZINGIRA KILICHOFANYIKA TAREHE 10.04.2017 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA

WALIOHUDHURIA

WAH: MADIWANI

1. Mh.Abdallah M. Nkane	- Nditi	- Mwenyekiti
2. Ally Nnunduma	- Mkuu wa Idara Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji	- Katibu
3. Mh.Ahmadi S. Makoroganya	- Ugawaji – Mwenyekiti H/W	- Mjumbe
4. Mh.Beatrice B. Lilungulu	- Mnero Ngongo Viti Maalum	- Mjumbe
5. Mh.Abilah S. Manyamba	- Naipingo	- Mjumbe
6. Mh.Abdalah A. Mkamate	- Kipara Mnero	- Mjumbe
7. Mh.Hamisi M. Nyasa	- Ndomoni	- Mjumbe
8. Mh.Saida Kata. Nahoma	- Nachingwea Viti Maalum	- Mjumbe
9. Mh.Lusia L. Mchopa	- Naipingo Viti Maalum	- Mjumbe
10. Mh.Emanuel Kata. Kinaki	- Matekwe	- Mjumbe
11. Mh.Gabriel D. Matuta	- Naipanga	- Mjumbe
12. Mh.Antony S. Lalo	- Namatula	- Mjumbe
13. Mh.Omari M. Lingumbende	- Namapwia	- Mjumbe
14. Mh.Joachim D. Nnungu	- Lionja	- Mjumbe
15. Mh.Emanuel A. Mhagama	- Namikango	- Mjumbe
16. Mh.Paulina S. Mchopa	- Stesheni	- Mjumbe
17. Mh.Hamida Matoroka	- Ngunichile Viti Maalum	- Mjumbe
18. Mh.Saada Y. Makotha	- Mkotokuyana	- Mjumbe
19. Mh.Hamisi M. Kalembo	- Mkoka	- Mjumbe

WATAALAM

1. Bakari M.Bakari	- Mkurugenzi Mtendaji (W)
2. Arbogast T.Kiwale	- Mtendaji Mkuu Mamlaka ya Mji Mdogo
3. Bihaga Yogwa	- Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala
4. Cesilia Kavishe	- Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
5. Ally Nnunduma	- Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji
6. Kenneth A.Mwangama	- Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
7. Lington Nzunda	- Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili
8. John D.Masika	- Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Zimamoto
9. Sarah E. Chiwanga	- Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
10. Mohamed H. Mnali	- Kaimu Afisa Biashara (W)
11. Jabir Ndagula	- Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki
12. Marko Mlungusye	- Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
13. Charles Chibwana	- Kaimu Afisa Ushirika (W)
14. Leornad D. Mkwela	- Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafishaji na Mazingira
15. Raphael Y.Ajetu	- Mkuu wa Idara ya Kilimo na Umwagiliaji
16.Humphrey Kambangwa	- Mratibu wa MIVARF
17. Shadrack S.Kaganga	- Mratibu wa Utawala Bora (W)
18.Daniel Bhoke	- Afisa Ardhi
19. James Mbakile	- Mratibu wa TASAF
20. Juma Mkopi	- Mwandishi wa Mikutano
21. Martha Kambona	- Mwandishi wa Mikutano

HWN/UUM/MUHTASARI NA 35/2017 KUFUNGUA KIKAO

Katibu alianza kwa kuwaeleza wajumbe kuwa Kikao hicho kilikuwa ni Kikao cha kawaida cha Kamati ya Ujenzi, Uchumi na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017 baada ya maelezo hayo ya awali Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue Kikao. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika Kikao hicho na aliwaeleza wajumbe kuwa Kikao hicho ni kwa ajili yao kuhoji na aliwajuza wajumbe kwamba Waheshimiwa Madiwani watatu(3) walishindwa kuhudhuria Kikao hicho kutokana na dharula,baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifungua Kikao saa 4: 22 Asubuhi.

HWN/UUM/MUHTASARI NA 36/ 2017 KUTHIBITISHA AJENDA

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kuzipitia ajenda za Kikao hicho, ambapo baada ya kuzipitia ajenda hizo wajumbe walizikubali kwa ajili ya kuzijadili.

HWN/UUM/MUHTASARI NA 36/ 2017 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 10.01.2017

Muhtasari ulisomwa na kupokelewa, Mwenyekiti na Katibu walitia saini zao kuthibitisha kuwa ni kumbukumbu sahihi ya Kikao hicho.

HWN/UUM/MUHTASARI NA 37/2017 YATOKANAYO

YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA UJENZI, UCHUMI NA MAZINGIRA TAREHE 10.01.2017

MUHT NA	AZIMIO	MTEKELEZAJI	UTEKELEZAJI
33/2017	1.Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara ahakikishe kuwa Chama Kikuu cha RUNALI kikaguliwe mauzo yote yaliyofanyanyika mwaka huu na wakibainika wanamakosa achukuliwe hatua za kisheria	Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara na Afisa Ushirika (W)	Kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Namba 6 ya mwaka 2013 kifungu Na 93(i),(2) na (3) inavitaka vyama kukaguliwa na COASCO au Mrajis wa Vyama vya Ushirika ngazi ya Mkoa. Aidha Ofisi ya Ushirika imekagua Vyama vya Msingi na kupata jumla ya Kgs 20,881,422 ndizo zilizouzwa na RUNALI kwa Wilaya ya Nachingwea na ushuru wote umelipwa kiasi cha Sh. 1,357,292,430.00
	2.Afisa Ushirika aandae taarifa ya mauzo ya korosho na kuwasilisha katika Mkutano wa Baraza la tarehe 27.01.2017	Afisa Ushirika (W)	Taarifa iliwasilishwa katika Mkutano cha Baraza la tarehe 27.01.217
	3. Taarifa ambayo Mh diwani wa Mkoka aliyokuwa nayo iwasilishe kwa Afisa Ushirika (W)	Afisa Ushirika (W)	Mpaka tarehe ya Kikao taarifa ilikuwa haijawasilishwa katika Ofisi ya Ushirika
33/2017	Matengenezo ya barabara wajumbe walikubaliana Mkaguzi wa Ndani afanye ukaguzi matengenezo ya Barabara Mianzini-Mnero miembeni,Mnero-Miembeni-Chikoko na Mkoka-Nandile bajeti ya 2015/2016 yenye gharama ya Sh. 198,870,000.00/=	Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani	Taarifa iliandaliwa na kuwasilishwa siku hiyo Kikaoni

Kamati ilipokea mrejesho wa yatokanayo na kikao kilichoagiza Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kifanye_ukaguzi matengenezo ya Barabara Mianzini-Mnero miembeni,Mnero-Miembeni-Chikoko na Mkoka-Nandile bajeti ya 2015/2016 yenye gharama ya Sh. 198,870,000.00/=.

Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa

HWN/UUM/MUHTASARI NA 38/2017 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA BARABARA KWA ROBO YA TATU MWAKA WA FEDHA MWAKA 2016/2017

Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Zimamoto aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya barabara kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 ambapo taarifa hiyo ilibainisha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea iliidhinishiwa kutumia jumla ya Sh.1,291,200,000.00 kwa ajili ya matengenezo ya barabara, ambapo Sh.975,150,000.00 kutoka Mfuko wa Barabara na Sh.316,050,000.00 ni kutoka Mfuko wa Maendeleo.Aidha kutokana na kuchelewa kuletwa kwa fedha za utekelezaji wa kazi za mwaka 2015/2016, utekelezaji wake uliendelea kufanyika katika mwaka wa fedha 2016/2017.Hadi kufikia tarehe 31/03/2017 Halmashauri ilipokea fedha jumla ya Sh.909,531,200.42 ambapo Sh.670,647,600.00 kati ya fedha hizo ni kwa ajili ya kulipa utekelezaji wa kazi mbalimbali za barabara kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 na Sh.238,883,600.42 zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za mwaka wa fedha wa 2016/2017.

Mwenyekiti wa Halmashauri alitoa ushauri kwa watumishi wa Sehemu ya Ushirika kwa kuwataka kuwa na busara na kuwasikiliza na kuwapokea pale wanapoenda kuhudumiwa katika ofisi ya Ushirika,aliendelea kusema kuwa ni muhimu kuwaeleza hali halisi iliyopo.

Uzidifu wa fedha,mjumbe alitaka kujua kuwa ni kwa nini RUNALI wasichukuliwe hatua kutokana na kuwasababishia vyama vya Ushirika hasara/makosa na wanashitakiwa wahasibu na hawana elimu ya utunzaji wa fedha. Baada ya mjumbe kutoa hoja alitoa ushauri kuwa wahasibu wa Vyama vya ushirika waajiriwe kwa mkataba na wawe wenye elimu ya utunzaji fedha.

Ufafanuzi; ulitolewa kuwa hoja imechukuliwa itafanyiwa kazi.

Iliazimiwa; kwamba Afisa Ushirika ahakikishe kuwa wahasibu wa vyama vya Ushirika wanakuwa na elimu ya utunzaji wa fedha na wasimamie upatikanaji kwa Bodi makini

Usajili wa vyama vya Msingi; mjumbe aliitaka Idara husika inayosimamia kutoa usajili wa vyama vya Msingi kuwa makini na Chama cha Msingi Matekwe.

Ufafanuzi; Wahusika wa Idara husika waliuchukua ushauri huo kwa utekelezaji.

Baada ya wajumbe wa Kamati ya Ujenzi, Uchumi na Mazingira kujadiliana kwa kina taarifa ya Ushirika wajumbe walitoa azimio kwamba baada ya kufanyika kwa uchaguzi wa Bodi za Vyama vya Ushirika, Afisa Ushirika (W) ahakikishe Bodi zinapata mafunzo.

HWN/UUM/MUHTASARI NA 47/2017 TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA SHUGHULI ZA IDARA YA USAFISHAJI NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI MACHI 2016/2017

Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafishaji na Mazingira aliwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa shughuli za Idara katika kipindi cha Januari -Machi 2017, kazi zilizotekelezwa ni usafishaji wa maeneo ya wazi, mifereji na barabara, usafirishaji wa taka ngumu toka kwenye vizimba na kuzipeleka dampo na kusimamia unyonyaji wa maji taka katika choo cha Shule ya Wasichana ya Nachingwea na Soko Kuu.

Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa.

HWN/UUM/MUHTASARI NA 54 /2017 KUFUNGA KIKAO

Katibu aliwashukuru wajumbe kwa uvumilivu waliouonyesha katika Kikao hicho na alisisitiza kuwa na imani kuwa wataalam waliyachukua maagizo,ushauri na maoni kwa ajili ya kufanyia kazi baada ya maelezo hayo mafupi Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge Kikao.Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa jinsi walivyoshiriki na kuchangia wakati wa kuzijadili ajenda ambapo alimkaribisha Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye alizungumza suala zima la Kituo cha Mabasi ambacho kilitakiwa kuanza tarehe 1.07.2017 kwa maagizo yalitolewa na Kamati ya Bunge na Kamati ya Bunge walipongeza kwa usimamizi wa miradi na kufikia hatua ya ukamilishaji,suala la maegesho ya magari kazi imetangazwa na Mkandarasi ameshasaini mkataba aliendelea kusema kuwa mradi wa Kitega Uchumi kinamaliziwa kutokana na Mkandarasi alikuwa anadai na ameshakwishalipwa.Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa usikivu waliouonyesha katika Kikao, baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifunga Kikao saa 8:09 Mchana.

UMETHIBITISHWA

.....

.....

KATIBU

.....

MWENYEKITI

19-09-2017

.....

TAREHE